SHULE YA UPILI YA MANGU

102/3
KISWAHILI
KARATASI 3
**KIDATO CHA NNE**
**FASIHI**
**MWIGO - 2022**
MUDA: SAA 2½

JINA: ____________________________________________

NAMBARI: ______________________ DARASA: ______________

<u>MAAGIZO</u>

i. Jibu maswali **<u>MANNE</u>**.
ii. Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
iii. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu **NNE** zilizobaki yaani; *Riwaya, Hadithi Fupi, Fasihi Simulizi na Tamthilia.*
iv. *Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*

| **SWALI** | A | B | | C | | D | | E |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** |
| **UPEO** | | | | | | | | |

**JUMLA =** 

*Fungua ukurara*

**SEHEMU YA A:** **SWALI LA LAZIMA**

1. **USHAIRI**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

*Akili zangu*
*Zasimama ufuoni*
*Macho yake*
*Yakikagua bahari.*
*Papa, mkali kama mauti*
*Anahangaisha samaki*
*Kwa ndaro na maringo*
*Daima akijigamba*
*Kwamba baharini*
*Haupo uwezo unaomtisha*
*Wala tisho linalomweza.*

*Wakati anaendelea kutiririka*
*Huku miongoni mwa samaki*
*Wingu zito la huzuni*
*Likizidi uzani.*

*Kama kwa sumaku*
*Samaki wanavutwa pamoja*
*Na nyuma ya ngao ya umoja*
*Wanaenda mwendo wa mbele*
*Wakiimba nyimbo zenye cheche.*

*Kwa hasira zenye moto*
*Papa anaongeza ukali,*
*Bali umati wa samaki*
*Haulegei muumano*
*Wala mwendo wa mbele*
*Kupungua kasi.*
*Mashambulizi makali*
*Ewaa! Mashambulizi!*
*Kutoka pande milioni*
*Dhidi ya papa muuaji.*

*Sasa baharini*
*Nyimbo za ufanisi*
*Zinapaa angani*
*Kama moshi wa ubani,*
*Na kubusu masikio*
*Kama muziki wa nyonza.*

---

***Maswali***

(a) Maudhui ya shairi hili yamegawanywa katika sehemu tatu. Zifafanue. (al. 3)

(b) Mbinu ya jazanda imetumika sana katika shairi hili. Thibitisha kwa kutoa mifano **mitano**. (al. 5)

(c) Onyesha mitindo mingine **minne** ambayo imejitokeza katika shairi hili. (al. 4)

(d) Tambua nafsi neni katika shairi hili. (al. 1)

(e) Jadili umuhimu wa aina **mbili** za urudiaji. (al. 2)

(f) Eleza umuhimu wa nidaa kama ambavyo imetumika katika shairi hili. (al. 2)

(g) Shairi hili linathibitisha toni kadhaa. Jadili ukweli huu kwa kutoa mifano **mitatu**. (al. 3)

**SEHEMU YA B: KIGOGO – PAULINE KEYA**

Jibu swali la 2 au 3

2. Wewe ni msichana mdogo hata ubwabwa wa shingo haujakutoka ila tu umenaswa katika utandu wa kasumba na flasafa za ukoloni mambo leo.

   (a) Yape maneno haya muktadha wake. (al.4)

   (b) Bainisha mbinu **mbili** za kimtindo ambazo zimetumika katika dondoo hili. (al. 2)

   (c) Kwa kumrejelea msemewa wa maneno haya; onyesha kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari. (al. 12)

3. (a) Badala ya viongozi wa Sagamoyo kuwasaidia wananchi kupiga hatua kimaendeleo wanazibomoa juhudi zao. Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi**. (al. 10)

   (b) Kufungwa kwa soko la Chapakazi kunawaathiri Wanasagamoyo vibaya. Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **kumi**. (al. 10)

**SEHEMU YA C: CHOZI LA HERI – ASSUMPTA MATEI**

Jibu swali la 4 au 5

4. (a) Wananchi katika riwaya hii wanasaidiana na kuinuana katika maisha. Jadili kweli wa kauli hii kwa kutoa mifano ishirini. (al. 20)

5. <u>**Soma kifungu hiki na kisha ujibu maswali**</u>

"Ni kweli asemavyo Tila," Ridhaa anayarudia maneno haya akilini, "mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Ukengeushi wa ardhi ukatiliwa muhuri, umilikaji wa ardhi na Waafrika katika sehemu hizi ukapigwa marufuku; si mashamba ya chai, si ya kahawa ... yote yakapata wenyeji wageni ... dau la Mwafrika likagonga jabali. Waafrika, akiwemo baba, Mzee Msubili, walilazimika kuwa, ama vibarua katika mashamba yaliyokuwa yao, au maskwota ambao maisha yao yalitegemea utashi wa Mzungu. Waafrika waliobahatika kuwa na makao yao binafsi walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao yenyewe; na bila shaka hali yao iliweza kutabirika; kuvyazwa kwa tabaka la wakulima wadogowadogo, maskini, wasio na ardhi. Nadhani unaweza kukisia hali ilivyokuwa kwa familia nyingi za Kiafrika. Kama vile Mzee Msubili alivyokuwa akisema, jamii yetu iligeuka kuwa hazina kuu ya wafanyakazi ambamo Wazungu wangeamua kuchukua vibarua kupalilia mazao yao. Vijulanga vilinyakuliwa kwa lazima kutoka kwenye susu zao, hata vifua havijapanuka, vinapelekwa katika maeneo mbalimbali nchini kufanya kazi."

"Hadi sasa hali hii haijabadilika, nakubaliana na Tila," Ridhaa alijiambia. "Ama hii ndiyo ile wanayoiita, *Historical Injustice*?" Ridhaa alimuuliza Tila mawazoni.

<u>**Maswali**</u>

(a) Changanua mitindo katika kifungu hiki. (al. 10)

(b) Kwa kutoa mifano <u>**kumi**</u>, tafanua zaidi maswala haya ambayo Ridhaa anayarejea kama historical injustice. (al 10)

## SEHEMU YA D: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

6. Jadili maudhui ya uwajibikaji kama ambavyo yamejitokeza katika hadithi ya Mwalimu Mstaafu. (al. 20)

7. <u>Soma kifungu hiki na ujibu maswali</u>

Maisha yangu hayakuwa maisha kitu tangia udogo wangu. Si maisha si wazimu! Mamangu Biti Kidebe naye alihitaji kulelewa. Daima alilalamika, "Miguu hii mie nitaingia nayo kaburini! Enh, miguu isiyosikia dawa, miguu gani hiyo?" Kilichobaki ikawa ni kuleana. Alinilea nami nikamlea.

Nilipokaramka nikaanza kujituma huku na huko. Nilijitahidi kutafuta vijikazi nilivyoviweza. Pengine nilichuma karafuu kwa kazi ya kibarua. Pengine nilimwangulia mtu nazi. Pengine nilienda pwani kurambaza au kuokota kombe na chanje. Pengine nilimsaidia mtu kijikazi chake mkono: kufyeka majani usoni pa nyumba yake, kuyachanja kuni magogo yake na hata kufua na kupiga pasi nguo zake. Kuna siku nilizochuma mabungo au zambarau au chocha au hata fuu kuuza. Nilichoambulia nilikipeleka nyumbani kitusaidie - mimi na mamangu. Hivyo hivyo, zikawa siku zinakwenda na umri unapungua.

Kwa upande wake mamangu alikuwa na mengi ya kufanya. Alijaribu kila alichoweza ili *tupone.* Akapika na kupakua tulichobahatisha. Maji yalipozidi unga alivikopoa viakiba vyake. Labda kweli: Jungu kuu halikosi ukoko. Lakini nilitambua pia maana ya akiba haiozi! Tulikuwa na vishamba tulivyopewa kulima. Viwili vya mpunga. Kimoja tulilima msimu wa mwaka, na kingine, msimu wa vuli. Kipande cha tatu tulilima mihogo na migomba miwili mitatu, japo migomba ya *bokoboko,* maana tangu hapo bokoboko si ndizi. Ingawa kuna wakataao kauli hiyo kwa kuiimbia nyimbo juu:

*Bokoboko ni ndizi,*
*Hasa likipata mpisi,*
*Na mpisi n' babu 'Amisi.*

Pamoja na yote lakini mamangu hakuacha kunitia skuli. Zama za elimu bure hizo. Kwa taabu na mashaka nikamaliza chumba cha nane. Kumaliza tu na mama akaenda jongomeo!...

(a) Changanua mitindo katika kifungu hiki. (al. 10)

(b) Jadili maudhui ya umaskini kama ambavyo yamejitokeza. (al. 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8.

*Umeanguka mwamba*
*Jabali tuloegemea*
*Lilotupa kimbilio*
*Mahasidi kutishia*
*Mti mkuu umegwa*
*Wana wa ndege wawapi?*
*Bila shaka hangaiko*
*'Metukumba makinda*
*Angalikuwa pamwe nasi*
*Maulana Mungu wetu*
*Swali hilo tungemuuliza*
*Mbona kaacha mauko*
*Ngome yetu kuvamia?*
*Ela mwenyewe Mwenza*
*Ajua hatima yetu*
*Lilobaki kumwamini*
*Riziki kutuangushia*

(a) Taja na ufananue muktadha ambao utungu huu unwaweza kutolewa. (al. 2)

(b) Taja sifa za ushairi simulizi ambazo zinazojitokeza katika utongo huu. (al. 5)

(c) Onyesha mitindo ambayo imetumika katika kifungu hiki. (al. 6)

(d) Umeamua kufanya utafiti wa kipera hiki kwa kushiriki.

i. Taja na ufafanue hasara zake. (al. 4)

ii. Taja na ufafanue faida zake. (al. 3)